SautiElimu

hakielimu

Toleo la 12
2006
ISSN 1821 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Je unautumia uhuru wako wa kutoa maoni?

Na Godfrey Telli, HakiElimu

Katika toleo hili tumechapisha maoni ya watu mbalimbali. Uhuru wa kila mtu wa kutoa maoni ni jambo la msingi katika demokrasia na haki za binadamu. Ni jambo la kuheshimiwa na kulindwa.

Siyo kila maoni yaliyomo humu ndani tunakubaliana nayo. Hata hivyo tunayaheshimu na kuyachapisha ili kila mmoja ayasome na kutoa mchango wake. Hii ndio dhana ya uhuru wa watu kutoa mawazo yao. Ibara ya 18 ya Katiba ya nchi yetu inahalalisha uhuru huu.

Voltaire, mwanafilosofia na mwandishi wa Kifaransa (1694-1778), aliwahi kusema: "I disapprove of what you say, but I will defend to the death your right to say it." Maana yake "Sikubaliani na unachokisema, lakini nitailinda haki yako ya kusema hivyo kwa nguvu zangu zote ikibidi hadi kifo".

Hapa tunajifunza nini? Kwamba uhuru wa kusema na kutoa maoni hautulazimishi kukubaliana na mawazo ya mwingine. Tunachotakiwa kukubaliana ni haki ya kila mmoja kutoa maoni yake bila kuwekewa vikwazo au visingizio. Yaani kukubaliana kutokukubaliana. Huu ndio msingi mkuu wa kukuza demokrasia yetu.

Hii haina maana kwamba ni sahihi kusema kitu chochote. Maneno ya uongo au yenye lengo la kuwadhuru wengine ni makosa. Kwa mfano maneno ya uchochezi Rwanda yalisababisha mauaji ya halaiki. Kusema kwa makusudi maneno ya uongo au uchochezi ni makosa. Ndio maana kila mmoja wetu anapaswa kutumia uhuru huu wa maoni kwa busara.

Kujenga au kukiuka misingi ya uhuru wa kutoa maoni huanzia katika familia. Kuna baadhi wanaoamini kwamba mkubwa akitamka jambo ni amri. Hii ni dhana potofu. Vilevile uhusiano kati ya mwalimu na mwanafunzi katika shule nyingi ni kwa mwalimu kutoa na mwanafunzi kupokea tu. Hii pia ni dhana potofu. Mzazi na mwalimu anatakiwa kuwasikiliza watoto na pia kujifunza kutoka kwao.

Tunaamini mabadiliko yatakuja. Yataanza na mimi na wewe. Wote tunaweza kuanza leo kuleta mabadiliko. Soma maoni yaliyomo. Pia tupe maoni yako ili wengine wayasome.

Ahsante na tunakutakia usomaji mzuri.

Je, unaijua Katiba yako?

Na Chambi Chachage, HakiElimu

Je, unajua kwamba kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake? Je, wewe unautumiaje uhuru huu? Ibara ya 18 ya Katiba ya nchi yetu inatamka bayana kwamba unao uhuru huu. Wengine wanautumia kwa kuchangia mawazo kwenye mikutano ya vijiji, mitaa, kamati na mabaraza ya shule. Wapo wanaoutumia kwa kuandika barua kwa wahariri wa magazeti. Jiulize: Je, nitautumiaje uhuru wangu wa maoni kwa kutoa mawazo yatakayoweza kuisaidia jamii yangu na kupanua demokrasia?

Je, unajua kwamba unayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari au taarifa bila kujali mipaka ya nchi? Hii nayo ni haki yako ya Kikatiba. Je, unautumiaje haki hii? Wapo watu wanaopeleka taarifa za vitendo vya rushwa kwenye vyombo vya dola kama vile Polisi na Taasisis ya Kuzuia Rushwa (TAKURU). Vilevile wapo watu wanaoitumia haki hii kutafuta ushauri wa kitaalamu kutoka kwenye taasisi mbalimbali kama vile UMATI na ANGAZA ili waweze kupambana na janga la UKIMWI. Ndugu msomaji jiulize: Je, nitaitumiaje haki yangu ya kupata na kutoa taarifa ili kuisadia jamii yangu iweze kupambana na rushwa, ujambazi na majanga?

Je, unajua kwamba kwa mujibu wa Katiba unao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yako? Je, unafaidi vipi matunda ya uhuru huu? Wengine wanautumia uhuru huu kuwasiliana na ndugu, jamaa na marafiki mbalimbali kwa ajili ya kujenga mahusiano ya kidugu na kimaendeleo. Wapo wanautumia uhuru huu kuwasiliana na vikundi mbalimbali kushirikiana navyo katika kuanzisha miradi mbalimbali ya kujiletea maendeleo. Jiulize: Je, ninaitumiaje haki hii katika kufanya mawasiliano yenye manufaa na yatakayosaidia jamii yangu katika kukuza uchumi wake na kupunguza umaskini?

Je, unajua kwamba unayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii? Katiba iko wazi kwamba hii ni haki yako. Je, unautumiaje? Wapo wanaoitumia kwa kusikiliza taarifa za habari na kusomba magazeti ili kupata ufahamu wa mambo muhimu yaliyojiri nchini na kwingineko. Wapo wanaokwenda kwenye ofisi za serikali za mitaa, vijiji na shule ila kupata taarifa za mapato na matumizi ya vijiji, mitaa na shule zao. Msomaji mpendwa jiulize: Je, naitumiaje haki hii kuomba na kufuatilia taarifa zinazoweza kunisaidia mimi binafsi, familia yangu na jamii kwa ujumla katika maisha yetu ya kila siku?

Shule ni nini?

Na Mwalyego Majid Shitambala, Dar es Salaam

Wananchi tulio wengi tunadhani maana ya shule ni majengo.

Hili ni kosa. Kutokana na pesa za ruzuku na michango ya wanajamii wananchi wengi wameamua kujenga shule nyingi za sekondari na kufurahia mafanikio hayo. Ninawapongeza kwa hilo. Lakini kitu kimoja ambacho hawajakigundua ni kiwango cha elimu kuzidi kushuka na watoto wengi wanakosa ari ya kwenda shule.

Fikiria mfano halisi: Katika mji mmoja kusini mwa Tanzania ilijengwa shule moja ya sekondari kwa nguvu za wananchi. Lakini ikaanza kutumika kabla ya kupata hadhi ya kuitwa shule kamili. Walimu walikuwa hawatoshi, haikuwa na maabara, vitabu hakuna na kwa ujumla mazingira yote ya shule hayakuandaliwa vizuri kuwapokea wanafunzi.

Ajabu ni kwamba, pamoja na matatizo yote katika shule hiyo, kipindi kifupi baadaye wananchi walihamasishwa tena na kuanza kujenga shule nyingine katika eneo hilo hilo! Wanafunzi wakapokelewa na masomo yakaanza kabla shule kukamilika! Shule hii ikawa na matatizo mengi, tena zaidi ya shule ya kwanza.

Muda mfupi baadaye ikajengwa tena shule nyingine ya tatu katika eneo hilo hilo! Bado ujenzi unaendelea katika shule hii. Na ujenzi ukikamilika wanafunzi wataanza kupokelewa kabla ya shule kukamilika.

Mimi naona kwa mtindo huu shule hizi haziwezi kutoa elimu bora hata kidogo. Tutajivunia tu kuwa na shule nyingi za sekondari katika eneo moja ambazo kimsingi si shule timilifu. Kwa nini wasikamilishe shule moja kabisa, na vifaa vyote vya kufundishia viwepo ndipo waanze kujenga shule nyingine? Na kwa nini shule hizi zisijengwe katika maeneo yaliyo mbali mbali kidogo?

Ningeomba kama kuna mahali ambapo wananchi wameanza kujenga shule; wahakikishe kwanza shule moja inakamilika kwanza. Ndipo waanze ujenzi wa shule nyingine. Na sio kukamilika kwa majengo tu. Shule ni pamoja na walimu, wanafunzi, maabara, vitabu na vifaa vingine vya kufundishia. Shule si majengo pekee!

Kiswahili kitumike kufundishia shule za msingi nchini

Na Lekta Burra, Mbulu, Manyara

Napenda kutoa maoni yangu kuhusu mfumo wa elimu ya msingi nchini ambao unabadilika mara kwa mara.

Wizara ya Elimu imebadili mambo mengi katika mitaala na lugha ya kufundishia. Mimi ningependelea lugha ya Kiswahili itumike kufundisha watoto wa shule za msingi. Hii ni kwa sababu lugha ya Kiingereza kisheria ni lugha ya pili baada ya Kiswahili. Lakini ukweli ni kwamba kiuhalisia hii si lugha ya pili kwa walio wengi bali ni lugha ya tatu.

Hebu jaribu kumfikiria mtoto huyu; yupo darasa la kwanza, umri wake ni miaka saba na anasoma katika shule ya msingi iliyopo kijijini. Je huyu atawezaje kufundishwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza? Lugha ya kwanza ya mtoto huyu aghalabu si Kiswahili bali ni lugha ya asili ya kabila lake. Je, Kiingereza ambacho kwake ni lugha ngeni kabisa ataelewa kitu kweli?

Kwa ufupi Tanzania inazo lugha nyingi za makabila zinazotumiwa na watu wengi vijijini. Watoto wengi wa vijijini wanazitumia lugha hizi kuwasiliana na katika shughuli zao za kila siku. Hivyo kuwafundisha watoto hawa kwa kutumia Kiingereza ni kuwadidimiza kielimu na kimtizamo wa kimazingira.

Suala la mazingira ya Kitanzania lipewe kipaumbele katika kuchagua lugha ya kufundishia, hususan katika shule za msingi. Kwa sababu hiyo basi Kiswahili kitumike. Nitafurahi wasomaji wa SautiElimu wakinichangia maoni zaidi kuhusu suala hili pamoja na la mitaala.



SautiElimu

Toleo la 12
2006
ISSN 1821 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Barua kwa SautiElimu

Shule za binafsi ziondoe kero hizi

Na Benedict G. Mahembe, Arusha

Nimejitahidi kufanya utafiti kidogo katika baadhi ya shule za binafsi hapa Arusha mjini na kugundua matatizo mengi yanayopaswa kurekebishwe. Shule nyingi kati ya hizi hutumia kiingereza kama lugha ya kufundishia kuanzia shule za awali hadi sekondari.

Baadhi ya shule hizi hazina walimu wenye taaluma ya ualimu. Kutokana na tatizo hili watoto hawapati elimu bora kulingana na malipo ya ada inayotolewa na wazazi. Pia ushirikiano kati ya walimu hawa na wazazi huwa ni mdogo sana, hususan mzazi anapokwenda kuulizia maendeleo ya mwanae.

Walimu hawa, pamoja na kukosa taaluma ya ualimu, hawatumii juhudi za kutosha katika kuhakikisha watoto wanapata elimu bora. Hawamsaidii mwanafunzi mwenye uwezo mdogo wa kuelewa masomo kwa haraka kulinganisha na wenzake. Badala yake huzingatia zaidi masomo ya ziada (tuition) ili kujiongezea kipato.

Wazazi wanapopeleka malalamiko yao kwa uongozi wa shule hakuna hatua zozote za maana zinazochukuliwa. Hapa tunabaki kujiuliza, je tunapozungumzia elimu bora kwa watoto wote wa nchi hii hawa wenzetu wanalichukuliaje suala hili?

Kamati ziweke bajeti za shule wazi

Na Hassan H. Hassan, Zanzibar

Kuna jambo moja ambalo linanisikitisha. Kwamba kamati nyingi za shule hazifahamu majukumu yao. Kwa mfano hapa kwetu sijawahi kusikia hata siku moja kamati yoyote ya shule ikitangaza hadharani bajeti yake ya shule. Wanachofanya ni kutangaza mipango yao ya maendeleo tu. Kwa nini wanashindwa kutangaza bajeti na mipango ya maendeleo ya shule kwa pamoja?

Majukumu ya kamati za shule ya kusimamia kwa uhakika na uangalifu mapato na matumizi ya shule hayatekelezwi kikamilifu. Kwa mfano, ukiwauliza hadi sasa kuna kiasi gani cha fedha na kuna mipango gani ya kuzitumia hawakupi jibu linaloeleweka. Wanatuambia 'pesa zenu zipo na hazijapotea. Msiwe na wasiwasi'

Hata katika kikao cha mwaka kati ya kamati ya shule na wazazi inakuwa vigumu kufahamu bayana kiasi cha fedha kilichopo, makusanyo na matumizi. Wanakamati wamekuwa wagumu sana kuweka mambo haya bayana.

Nazishauri kamati za shule ziwe wazi zaidi. Watangaze mapato na matumizi kwa kipindi kilichopita, kipindi cha sasa na kipindi kijacho kwa wazazi, walimu na wanafunzi. Hali hii itaamsha ari ya wananchi kujitolea na kuongeza michango. Wananchi pia watakuwa na uhakika kwamba wanachokitoa kinatumika kama ilivyokusudiwa. Pia wataongeza imani kwa kamati ya shule na kuondokana na dhana kwamba baadhi ya wanakamati si waaminifu.

Elimu ya msingi iboreshwe zaidi

Na Edward Moses, Arusha

Mimi ni mwalimu wa shule ya msingi. Napenda kutoa dukuduku langu ili kuboresha elimu ya msingi. Ukweli ni kwamba pamoja na kuwepo kwa majengo mazuri katika shule nyingi za msingi nchini, bado kuna masuala mengi yanayopaswa kuzingatiwa ili kuboresha elimu zaidi.

Madawati, idadi ya kutosha ya walimu wenye motisha, na vifaa vya kufundishia na kujifunza ni baadhi tu ya mahitaji muhimu yanayopaswa kupewa kipaumbele.

Napenda kukiri wazi kwamba nchi yetu ni kubwa kijiografia na shule nazo ni nyingi sana. Hata hivyo matatizo niliyoyataja tunaouwezo wa kuyatatua na kuzifanya shule zetu kuwa na ufanisi wa kutosha.

Pesa inayotolewa na Serikali haitoshelezi na walengwa hawajui muda wala kiwango watakachogawiwa. Na hata kama itatosheleza na kutolewa kwa wakati bado si kigezo pekee cha kutatua matatizo ya elimu shuleni.

Hebu fikiria shule ya msingi yenye wanafunzi zaidi ya 500 ina walimu 7 tu! Katika hali hiyo tunatarajia nini? Hapa tunagundua kwamba upungufu wa walimu bado ni tatizo kubwa sana. Pamoja na upungufu kuwa tatizo maslahi yao hayashughulikiwi kama ilivyotarajiwa.

Marekebisho ya mishahara ya walimu baada ya kupanda daraja hayafanyiki kwa wakati. Fedha za uhamisho wao ama hazipatikani kwa wakati au hazipatikani kabisa. Hali hii huwakatisha tamaa walimu na kuwalazimisha kujiingiza katika shughuli nyingine za kibinafsi badala ya masuala ya kitaaluma.

Tutawasaidiaje walimu kufundisha vizuri zaidi?

Mercy Charles Masasi, Dar es Salaam

Walimu wanaweza kufundisha vizuri zaidi kama watapata mishahara mizuri, yenye kutosheleza mahitaji yao na familia zao.

Walimu wanaweza kufundisha vizuri kama watawekewa mazingira mazuri ya kufundishia. Mazingira hayo ni pamoja na kujengewa nyumba karibu na shule ili kuepuka uchovu wa safari ndefu hadi shuleni.

Pia idadi ya wanafunzi katika darasa moja iwe ya wastani na si kubwa sana ili kumwezesha mwalimu kufundisha vizuri. Hapo mwalimu pia ataweza kuwafuatilia wanafunzi wake kwa ukaribu na urahisi zaidi.

Walimu wanahitaji kutiwa moyo kwa namna mbalimbali kama vile kutoa zawadi kwa mwalimu bora, kusikilizwa pale wanapokuwa na shida na kusaidiwa kutatuliwa matatizo yanapowakabili.

Shule hazifaulishi

Agness Michael, Mawenzi, Morogoro

Kuna baadhi ya shule za msingi ambazo hazifaulishi watoto kwenda sekondari kwa muda mrefu. Unakuta shule haitoi mtoto hata mmoja kwenda sekondari kwa mfululizo hadi miaka mitano.

Hali hii inawavunja moyo sana wanafunzi wengine wa madarasa ya chini waliopo shule hiyo. Wanakosa matumaini ya kuendelea na masomo ya sekondari. Kwa kweli hapo elimu haiwezi kuboreka.

Serikali za vijiji/mitaa zilivalie njuga suala hili ili kugundua matatizo na kuyapatia ufumbuzi. Pia kuwepo na utaratibu wa kuamisha walimu mara kwa mara. Labda hali inaweza kuboreka, kwani walimu kukaa mahali pamoja muda mrefu inaweza kuwa ni sehemu ya tatizo.

Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania

Kila mtu:

a) anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake;

b) anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi;

c) anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na

d) anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki na demokrasia katika elimu na jamii. Tunafanya hivyo kwa kuwezesha jamii kupata habari, kubadili shule na kfumo wa uundaji wa sera; kuchochea ubunifu wa mijadala ya umma; kufanya utafiti yakinifu, uchambuzi wa sera na utetezi na kushirikiana na wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Shukrani kwa PANOS kwa picha na kwa wote walioandaa habari zilizochapishwa katika jarida hili.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya jarida hili kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chazo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala mbili kwa HakiElimu.

Mhariri Mkuu:
Rakesh Rajani

Timu ya SautiElimu
Godfrey Telli na
Robert Mihayo

Tuandikie!

HakiElimu SautiElimu
S.L.P. 79401
Dar es Salaam Tanzania
Simu: (022151852 au 3
Fakisi: (022152449
Baruapepe: media@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

ISSN 1821 5072

© HakiElimu 2006

Pata nakala yako ya bango la Mkukuta sasa. Tuandikie!

Ukurasa wa 2